

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي مَشْرُوعُ تَعْلَمُ الْإِسْلَامَ – أصول العقيدة - سواحيلي

Samo la 6

الدرس السادس

MASHARTI YA KALIMA YA LAAILAAHA ILLALLAH.

Kalima ya LAAILAAHA ILLALLAH inayo masharti saba, haifai mpaka yakusanyike masharti yote pamoja, na ashikamane nayo mtu bila ya kuacha hata sharti moja miongoni mwa masharti hayo ni;

1. Elimu (kujua) nayo maana yake ni kukataa na kuthibitisha nay ale yanayo lazimika kuyafanyia kazi, atakapo elewa mtu kuwa Allah (sw) ndiye anayestahiki kuabudiwa pekee, na kwamba ibada yoyote ifanywayo kinyume ya Allah ni batili haifai, basi mtu huyo atakuwa ameifahamu maana halisi ya hili neno la LAAILAAHA ILLALLAH.

قال تعالى: ﴿فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ﴾ [محمد: ١٩].

Allah (sw) anasema : ("Basi tambua na kujua ya kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Allah peke yake") (Muhammad:19).

Hadithi ilipokelewa na Othman (Radhiyaaalahu Anhu), Mtume (saw) anasema :

وعن عثمان رضي الله عنه، عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: ((من مات وهو يعلم أنه لا إله إلا الله دخل الجنة)) [مسلم: ٢٦].

(" Yeyote atakaekufa hali yakuwa anajua ya kwamba hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah pekee ataingia peponi") (Amepokea Imamu Muslim).

2. Yakini , ni pale mtu kuitamka shahada kwa yakini iliyotulia moyoni mwake, bila ya kuingiwa na shaka inayowekwa na shetani wa kijini au wa kibinadamu, bali aiseme shahada akiwa na yakini ya kisawasawa.

قال الله تعالى: ﴿ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا ﴾ [الحجرات: ١٥].

Allah (sw) anasema : (" Hakika si vinginevya waumini wa kweli ni wale ambao wamemuamini mwenyezi mungu na mtume wake, kasha wakawa hawana shaka yoyote") (Al-hujrat :15).

وعن أبي هريرة - رضي الله عنه - أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: ((أشهد أن لا إله إلا الله و أني رسول الله، لا يلقى الله بها عبدٌ غيرَ شاكٍّ فيها،

إلا دخل الجنة)) [مسلم: ٢٧].

Hadithi aliyoipokea Abu Huraita Radhi za Allah ziwe juu yake, Mtume (saw) anasema: ("Mwenye kushuhudilia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na akushuhudilia ya kwamba mimi ni mtume wa Allah, akawa mtu si mwenye shaka juu ya maneno mawili haya, isipokuwa ni kuingia peponi") (Ameipokea Imamu Muslim).

3. Kukubalika ni kuwa ukubali moyo na ulimi wake mtu kwamba kila ambacho kimeamuriwa na neno hili, basi asadikishe kwa kuelezwa, aamini kwa kila kilichokuja kutoka kwa Mtume (saw), na ayakubali hayo yote bila ya kuacha chochote kutoka kwake mtume (saw), Allah (sw) anasema:

قال الله تعالى: ﴿ آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفِرُّ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴾ [البقرة: ٢٨٥].

("Ameamini mtume wa mwenyezi mungu, yale aliyoletewa kwa njia ya wahyi kutoka kwa mola wake, na waumini pia wameamini, kila mmoja katika wao amemuaamini mwenyezi mungu ya kuwa ana malaika, ameteremsha vitabu na ametuma mitume, na hatukanushi yeyote katika mitume bali tunawaamini wote, na wanasema tumesikia na tumetii, tunatarajia msamaha wako mola wetu, na kwako pekee ndio marejeo") (Al-Baqarah :285).

Na hayatakubaliwa kwa yule ambae atapinga baadhi ya hukumu za kisheria, kama vile kusimamisha hukumu ya haddi kwa wale ambao walioiba, kuzini, kupinga mtu kuoa wake Zaidi ya mmoja, kupinga mirathi ya kiislamu na mengi mengineyo ya kisharia.

قال تعالى: ﴿ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ﴾ [الأحزاب: ٣٦].

Allah (sw) anasema :("Haipaswi kwa muumini wa mwanaume wala muumini mwanamke, iwapo mwenyezi mungu na mtume wake wametoa uamuzi wataenda kinyume nao") (Al – Ahzab : 36).